# Je Wewe ni Mtetezi wa Uwazi wa Mikataba?

*Uwazi wa Mikataba ni kuhusu kuufanya mchakato wote wa utayarishaji wa mikataba kuwa wazi, wa haki, na wenye ufanisi: tokea hatua za upangaji, utoaji wa zabuni, ugawaji linganifu, na utoaji wa mikataba hadi utekelezaji*

*"Kufanikiwa Kuwa na Serikali Yenye Uwazi Kunahitaji Nchi Iweke Mifumo na Mipango Inayohitaji Kuakisiwa Katika Sera, Sheria na Taasisi za Taifa."*
**Jakaya Kikwete**

## Usuli

Mikataba inayoingiwa kati ya mataifa yenye utajiri wa rasilimali na makampuni ya kimataifa ni ya muhimu kwa kuwa inaeleza waziwazi, wajibu, manufaa, haki na usalama katika uwekezaji kwenye mafuta, gesi na uchimbaji madini. Kwa miongo mingi sasa, uwekwaji wazi wa mikataba ya uchunguzi na uchimbaji wa rasilimali (hasa madini, mafuta na gesi asilia) nchini Tanzania umebaki kuwa ni TATIZO KUBWA. Kutoweza kuona mikataba hiyo kunazuia wananchi wasiweze kupata taarifa sahihi, kunapunguza hali ya kujiona kuwa ni wamiliki wa rasilimali zao na kunapunguza ari na uwezo wao wa kusoma kwa uangalifu na kushiriki kikamilifu katika majadiliano au maamuzi kuhusu jinsi nchi inavyopaswa kusimamia rasilimali zake. Uwazi wa Mikataba ni kuhusu kuufanya mchakato wote wa utayarishaji wa mikataba kuwa wazi, wa haki, na wenye ufanisi: tokea hatua za upangaji, utoaji wa zabuni, ugawaji linganifu, na utoaji wa mikataba hadi utekelezaji.[1]

## Uwazi wa Mikataba Nchini Tanzania

Taasisi kuu inayowajibika kwa viwango na taratibu za ununuzi wa umma na inayofuatilia mashirika/taasisi za ununuzi wa umma kama zinafuata kanuni zilizowekwa ni Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA). Shirika la Huduma za Manunuzi ya Serikali (GPSA) hufanya ununuzi wa jumla kwa makadirio ya mahitaji ya taifa kwa lengo la kuuza tena kwa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali. GPSA huchapisha data za manunuzi katika tovuti yake kwa muundo wa data za wazi.

Serikali ina wajibu wa kuwa wazi na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika huduma za manunuzi na utoaji wa mikataba; lakini, hakuna mpango ulio wazi wa kushirikisha wananchi na sekta binafsi katika suala zima la Uwazi wa Mikataba.

Zaidi ya hayo, mfumo wa kisheria unaoongoza PPRA hautoshelezi. Marekebisho ya sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2016, yana madhumuni ya kushughulikia mapengo ya kisheria ikiwa ni pamoja na uwekaji wazi wa mikataba. Sheria iliyorekebishwa inataka kuwe na shahidi wakati wa kutia sahihi mikataba, na kwa vyombo/taasisi husika kutoa taarifa za manunuzi kwa njia ya kielektroniki (inapowezekana) au kwa mkono. Serikali pia ilipitisha sheria nyingine zenye uhusiano na uwekaji wazi wa taarifa kama vile Katiba ya Tanzania ambayo inaruhusu uhuru wa habari; Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari na Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa, 2016 ambazo hutoa haki kwa wananchi kupata taarifa zilizohodhiwa na serikali. Sheria hizi hazitoshi kwani zina baadhi ya vipengele vinavyozuia kupatikana kwa baadhi ya taarifa kwa hiyo, Sheria ya Manunuzi ya Umma ya 2016 kwa mfano, inatakiwa iguse na maeneo mengine zaidi ya kuwa na shahidi, ishughulikie suala la uwekaji uwazi wa mikataba.[2]

## Kwa Nini ni Muhimu Katika Sekta za Mafuta, Gesi Asilia na Uchimbaji Madini Tanzania?

Ikiwa ni nchi iliyoridhia mpango wa EITI tangu mwaka 2012, utekelezaji wake Tanzania na sheria ya TEITA, ya mwaka 2015 hadi sasa ndiyo zana muhimu zinazowezesha wadau, hasa watunga sera kufuatilia na kusimamia menejimenti ya serikali kwa mikataba ya uziduaji. Lakini kwa hakika nchi **imeshindwa** kutimiza ahadi na wajibu wake kuhusu uwekaji wazi mikataba, na kuiacha iwe ni fumbo kwa wadau.

[1]https://www.open-contracting.org/wp-content/uploads/2016/02/OCP2016_EITI_brief.pdf
[2] Open Contracting Data Programme of Hivos: https://hivos.org/focal-area/open-contracting

Serikali iliyo wazi na yenye kuwajibika hujenga uwezo wa mwananchi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa utoaji maamuzi na kutoa mchango chanya katika mapato yanayozalishwa. Hili linawezekana kufaulu pale tu mipango ya uwekezaji ya serikali itaendeshwa kwa uwazi na wananchi na wadau husika kuweza kuchunguza kwa umakini.

Matakwa ya umma ni kuelewa jinsi rasilimali zao zinavyogawanywa na kutumiwa. Kufanikisha hili, wananchi lazima wapashwe habari kuhusu utayarishaji wa mikataba ya umma; muundo wa uendeshaji shughuli, mapato, tathmini ya matokeo kwa mazingira, mgawanyo wa mapato, na ushiriki wa wananchi. Kwa sababu hii, uwekaji wazi wa nyaraka zinazotokana na sekta ya uziduaji kama sehemu ya mchakato wa manunuzi ni kipengele muhimu cha Serikali Iliyo wazi.

## Wapi Watunga Sera Wanaweza Kuongoza Msukumo wa Kuboresha Mfumo wa Taratibu za Kisera na Udhibiti Kuhusu Uwazi wa Mikataba Nchini:

Watunga sera wanaweza kutumia nafasi waliyopewa kuboresha uwazi kupitia uwekwaji wazi mikataba kwa sababu zifuatazo:

- Haki kwa wote: Kusudi majadiliano ambayo serikali itaingia na makampuni ya kimataifa yafanyike kwa kuzingatia haki na usawa kwa pande zote, na kwamba serikali na makampuni yanayowekeza waweze kunufaika kutokana na uwekezaji wao.
- Kujenga mahusiano na uaminifu: Kuhakikisha kuwa hakuna taarifa zinazopotea ili kufikia upeo wa manufaa yanayotokana na sekta. Upatikanaji wa mikataba hii, huongeza uelewa wa wadau (AZAKI na Umma) jambo ambalo hujenga hali ya kuaminiana kati ya jamii, serikali na makampuni.
- Ufanisi wa ufuatiliaji wa kanuni/sheria: Ushiriki wa watunga sera katika mchakato wa ufuatiliaji wa mfumo wa kisheria wa sekta ya uziduaji unasaidia kuhakikisha kuwa matarajio ya nchi hasa kuhusu hisa za serikali yanakuwa halisi. Uwazi wa Mikataba huwezesha kufahamu kama sheria na kanuni zilizowekwa zimetekelezwa na kuwawajibisha wahusika.

## Jinsi ya Kuongoza Msukumo?

Watunga sera wenye ufanisi ni muhimu sana kwa kuunda na kuhimiza Uwazi wa Mikataba na kuleta mafanikio. Mtunga sera anayeshiriki kikamilifu katika Uwazi wa Mikataba anaweza kujiweka katika mstari wa mbele wa kutoa sauti na kuongoza katika upatikanaji wa utawala bora na uwazi. Ifuatayo ni mifano ya jinsi mtunga sera anavyoweza kusaidi katika upatikanaji wa Uwazi wa Mikataba katika sekta ya uziduaji:

- Pigania upatikanaji wa sheria mahususi ya Uwazi wa Mikataba;
- Shawishi na tetea marekebisho ya sheria ya TEITA na kanuni zake ili iongezewe kipengele cha Uwazi wa Mikataba;
- Pigania uundaji wa jopo la watunga sera kuhusu Uwazi wa Mikataba;
- Jenga mahusiano na waandishi wa habari ili kuinua uelewa wa umma kuhusu Uwazi wa Mikataba na kuonyesha maeneo ambapo mchakato unaweza kuboreshwa;
- Omba taarifa kuhusu Uwazi wa Mikataba kutoka kwa AZAKI zinazojihusisha na masuala ya uziduaji;
- Eleza ushiriki wako katika suala la Uwazi wa Mikataba katika jimbo lako la uchaguzi ili kuimarisha uelewa wa wananchi na onyesha jinsi unavyoweza kuwa wa manufaa kwao; na
- Chochea utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yanayotokana na ripoti za EITI.

## Kinachohitajika Kufanikisha



**Thamani kwa Fedha**



**Kupungua kwa Wizi na Rushwa**



**Utekelezaji Bora Zaidi**



**Mazingira ya Biashara ya Haki Zaidi**

## Wasiliana na:

Policy Forum, S. L. P. 38486, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2780200 • Simu ya kiganjani: +255 782317434
Barua pepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum.or.tz

HakiRasilimali, S. L.P. 38486, Dar es Salaam, Tanzania
Simu ya kiganjani: +255 (0) 745 655 655
Barua pepe: info@hakirasilimali.or.tz
Tovuti: www.hakirasilimali.or.tz